

***KUMB: PPR/16 - 5/1***

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA  
JUMATANO, TAREHE 4 Mei 2016**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 4 Mei 2016**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepanda ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 6 Aprili 2016. Kwa Mwezi Mei 2016, bei za rejareja zimepanda kama ifuatavyo; Petroli Sh 57/lita sawa na asilimia 3.27, Dizeli Sh 86/lita sawa na asilimia 5.64 na Mafuta ya Taa Sh 76/lita, sawa na asilimia 5.07, sawia. Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita bei za jumla nazo zimepanda kama ifuatavyo; Petroli Sh 56.53/lita sawa na asilimia 3.49 Dizeli Sh 85.56/lita sawa na asilimia 6.08 na Mafuta ya Taa Sh 76.18/lita sawa na asilimia 5.47, sawia. Kwa kiasi kikubwa, mabadiliko haya yametokana na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia
- (b) Mamlaka inapenda kuujulisha umma ya kwamba bei hizi kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana vile vile kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (c) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (d) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo ziwe chini ya bei kikomo (price cap) kama ilivyokokotolewa na fomula iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 405/2015 la Mwezi Julai 2015.**
- (e) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (f) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama

kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

### A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/lita)	Mafuta Ya Taa (Sh/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	1,785	1,602	1,578
<b>Arusha</b>	1,869	1,686	1,661
Arumeru (Usa West)	1,869	1,686	1,661
Karatu	1,887	1,704	1,680
Monduli	1,874	1,691	1,667
Ngorongoro (Loliondo)	1,925	1,742	1,718
<b>Kibaha</b>	1,789	1,606	1,582
Bagamoyo	1,796	1,613	1,589
Kisarawe	1,792	1,609	1,585
Mkuranga	1,794	1,611	1,587
Rufiji	1,812	1,629	1,605
<b>Dodoma</b>	1,843	1,660	1,636
Bahi	1,851	1,668	1,644
Chemba	1,870	1,687	1,663
Kondoa	1,876	1,693	1,669
Kongwa	1,841	1,658	1,633
Mpwapwa	1,844	1,662	1,637
<b>Iringa</b>	1,849	1,666	1,641
Kilolo	1,853	1,670	1,646
Mufindi (Mafinga)	1,859	1,676	1,652
<b>Njombe</b>	1,877	1,694	1,670
Ludewa	1,915	1,732	1,708
Makete	1,908	1,725	1,701
Wanging'ombe (Igwachanya)	1,875	1,692	1,668
<b>Bukoba</b>	2,000	1,817	1,792
Biharamulo	1,974	1,791	1,767
Karagwe (Kayanga)	2,016	1,833	1,809
Kyerwa (Ruberwa)	2,022	1,839	1,815
Muleba	2,000	1,817	1,792
Ngara	1,965	1,782	1,758
Misenyi	2,008	1,825	1,801

<b>Geita</b>	1,950	1,767	1,743
Bukombe	1,939	1,756	1,732
Chato	1,971	1,788	1,764
Mbogwe	1,988	1,805	1,781
Nyang'hwale	1,965	1,782	1,758
<b>Kigoma</b>	2,016	1,833	1,808
Uvinza (Lugufu)	2,028	1,845	1,821
Buhigwe	2,005	1,822	1,798
Kakonko	1,973	1,790	1,766
Kasulu	2,002	1,819	1,794
Kibondo	1,980	1,797	1,773
<b>Moshi</b>	1,858	1,675	1,651
Hai (Bomang'ombe)	1,862	1,679	1,654
Mwanga	1,851	1,668	1,644
Rombo (Mkuu)	1,879	1,696	1,672
Same	1,845	1,662	1,637
Siha (Sanya Juu)	1,865	1,682	1,658
<b>Lindi</b>	1,843	1,660	1,636
Kilwa Masoko	1,818	1,636	1,611
Liwale	1,864	1,681	1,657
Nachingwea	1,873	1,690	1,665
Ruangwa	1,871	1,688	1,663
<b>Babati</b>	1,907	1,724	1,700
Hanang (Katesh)	1,917	1,734	1,710
Kiteto (Kibaya)	1,918	1,735	1,711
Mbulu	1,920	1,737	1,712
Simanjiro (Orkasumet)	1,939	1,756	1,732
<b>Musoma</b>	1,963	1,780	1,756
Rorya (Ingirijuu)	1,972	1,789	1,765
Bunda	1,954	1,771	1,747
Butiama	1,960	1,777	1,753
Serengeti (Mugumu)	2,008	1,825	1,801
Tarime	1,974	1,791	1,767
<b>Mbeya</b>	1,892	1,709	1,684
Chunya	1,901	1,718	1,694
Ileje	1,905	1,722	1,697
Kyela	1,907	1,724	1,700
Mbarali (Rujewa)	1,876	1,693	1,669
Mbozi (Vwawa)	1,901	1,718	1,694
Momba (Chitete)	1,910	1,727	1,703
Rungwe (Tukuyu)	1,901	1,718	1,693

<b>Morogoro</b>	1,810	1,627	1,602
Mikumi	1,825	1,642	1,618
Kilombero (Ifakara)	1,847	1,664	1,640
Ulanga (Mahenge)	1,858	1,675	1,651
Kilosa	1,828	1,645	1,621
Gairo	1,828	1,645	1,621
Mvomero (Wami Sokoine)	1,820	1,637	1,613
Turian	1,835	1,652	1,628
<b>Mtwara</b>	1,857	1,674	1,650
Nanyumbu (Mangaka)	1,906	1,723	1,699
Masasi	1,883	1,700	1,675
Newala	1,889	1,706	1,682
Tandahimba	1,882	1,699	1,675
<b>Mwanza</b>	1,934	1,751	1,727
Kwimba	1,971	1,788	1,763
Magu	1,942	1,760	1,735
Misungwi	1,940	1,757	1,733
Sengerema	1,967	1,784	1,760
Ukerewe	1,994	1,811	1,787
<b>Sumbawanga</b>	1,957	1,774	1,750
Kalambo (Matai)	1,950	1,767	1,743
Nkasi (Namanyeale)	1,971	1,788	1,764
<b>Katavi (Mpanda)</b>	1,992	1,809	1,785
Mlele (Inyonga)	1,971	1,788	1,763
<b>Songea</b>	1,908	1,725	1,701
Mbinga	1,941	1,758	1,734
Namtumbo	1,937	1,754	1,730
Nyasa (Mbamba Bay)	1,944	1,761	1,737
Tunduru	1,967	1,784	1,759
<b>Shinyanga</b>	1,913	1,730	1,706
Kahama	1,927	1,744	1,720
Kishapu	1,942	1,759	1,735
<b>Simiyu (Bariadi)</b>	1,955	1,772	1,748
Busega (Nyashimo)	1,948	1,765	1,741
Itilima (Lagangabilili)	1,958	1,775	1,751
Maswa	1,946	1,763	1,739
Meatu (Mwanhuzi)	1,953	1,770	1,746
<b>Singida</b>	1,875	1,692	1,668
Iramba	1,887	1,704	1,680
Manyoni	1,860	1,677	1,653
Ikungi	1,871	1,688	1,664

Mkalama (Nduguti)	1,900	1,717	1,693
<b>Tabora</b>	1,939	1,756	1,731
Igunga	1,893	1,710	1,685
Kaliua	1,957	1,774	1,750
Ulyankulu	1,951	1,768	1,744
Nzega	1,903	1,720	1,696
Sikonge	1,950	1,767	1,743
Urambo	1,952	1,769	1,744
<b>Tanga</b>	1,688	1,507	1,624
Handeni	1,709	1,527	1,603
Kilindi	1,724	1,542	1,638
Korogwe	1,700	1,519	1,617
Lushoto	1,710	1,528	1,626
Mkinga (Maramba)	1,695	1,514	1,638
Muheza	1,693	1,511	1,624
Pangani	1,695	1,513	1,630

**B: BEI ZA JUMLA**

<b>Bei za Jumla - DSM</b>	<b>Petroli (Sh/L)</b>	<b>Dizeli (Sh/L)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Sh/L)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>1,676.68</b>	<b>1,493.74</b>	<b>1,469.50</b>

<b>Bei za Jumla - TANGA</b>	<b>Petroli (Sh/L)</b>	<b>Dizeli (Sh/L)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>1,580.18</b>	<b>1,398.56</b>

**Felix Ngamlagosi**

**MKURUGENZI MKUU  
EWURA**